UK 14

# Uwekezaji bidhaa za ngozi itakavyochochea ajira kwa vijana, mapato

ngozi, kwa sababu waliopo ni wachache na hawana ujuzi wa kutosha," alisema Woiso.

> *Serikali iwekeze zaidi katika kutoa elimu kwa vijana wanaotaka kufanya kazi katika sekta ya ngozi, kwa sababu waliopo ni wachache na hawana ujuzi wa kutosha ...*
>
> **Keneth Woisso**
> Mjasiriamali wa ngozi

Tanzania na Misri zimeanza mikakati ya uwekezaji katika sekta ya ngozi nchini, ambapo Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alikutana kufanya mazungumzo na wawekezaji kutoka nchi hiyo ambao walifika nchini kwa nia ya kuwekeza katika sekta hiyo.



**Baadhi ya vijana nchini wakiwa katika shughuli za uzalishaji bidhaa zitokanazo na ngozi.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned by CamScanner

...wa kuhudhuria waweze

kupuuzia mambo.

alisema hiki ni kipindi ambacho Watanzania wanatakiwa

na kuangalia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

MAJIRA UK 9



**Mkurugenzi wa Uzalishaji Mifugo na Masoko, Dkt. Felix Nandonde akihimilisha ng'ombe mmoja kama uzinduzi wa zoezi la kuendeleza makambi ya uhimilishaji wa ng'ombe lililofanyika katika Kijiji cha Kazibizyo Kata ya Ng'anzo Wilaya ya Bukombe Mkoa wa Geita.** (Na Mpigapicha Wetu)

na Mfuko wa
sh. milioni 94
shughuli zao
kiuchumi.
Akizungum
karibuni Mku
cha Ufugaji
Halmashaur
hiyo, Seif S
vikundi hivy
ili kuongeza
mazao ya n
mapato ya
Alitaja vi
kiasi walich
Environme
and Bee K
Akinaman
Akinaman
Inala Beek
Environme
Group.
Kikundi
Initiative E
vikundi hi
Kata za It
Ndevelw
Salum
hivyo vili
mwaka v
kwa leng
za ufuga
zilitumik
ya kisas
mabanc
kujenga
kutolea
Alise
cha ku
hayo c
kimear
katika
tayari,
Shirika

a wavuvi wa
ko Uganda
iwa kuwa ni
a Uganda n
ma Tanzania
a uendeshaji
sema wao
nasafirisha
va freshi na
wanazuia
abo lakini
a mfano
do wilaya
sh. 4,000
vabaishara
li mzigo
ema Dkt.
a samaki
ko la ajira
Mjumbe
a Bunge
i Pascal
eria za
chi kwa



# *Serikali kuwasaidia wawekezaji NARCO*

**Na Ashura Jumapili, Missenyi**

■■SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo tayari kuwasidia wawekezaji wazawa waliowekeza katika Ranchi za Taifa (NARCO) kupata mikopo katika taasisi za fedha kwa kutumia mifugo yao ili waweze kufanya uwekezaji wenye tija na kuinua sekta hiyo. Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Kilimo na Mifugo, Abdallah Ulenga mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo,Mifugo na Maji iliyo tembelea MARCO wilayani Misenyi na kuzungumza na wawekezaji hao wazawa waliowekeza eneo hilo.

Ulenga alisema miaka yote wafugaji wanashindwa kukopa kwa sababu mifugo haipokelewi kama dhamana katika taasisi mbalimbali za mikopo.

Alisema kutokana na Serikali kutoa kipaumbele kwa wawekezaji wazawa kuwekeza katika Ranchi za Taifa wizara hiyo imekutana na benki ya maendeleo ya kilimo (TADB) ili kuweka mikakati ya pamoja ya kuwakopesha wafugaji hao.

Awali kabla ya kukutana na wawekezaji hao katibu mkuu wa Wizara ya Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel,alisema Mkoa wa Kagera una ranchi tano ambazo ni Missenyi, Kagoma,Mabale,Kikulura na Kitengure zinazosimamiwa na NARCO na Ranchi moja ya Missenyi inakilometa za Mraba zaidi ya 60,000 na ngíombe zaidi ya 1,900.

Alitaja mikakati ya Wizara kuwa kwa kushirilikiana na NARCO, Ranchi zote za taifa zinaendelea kuwekewa miundombinu salama ,kujenga majosho ,kuendelea kuhamasisha wawekezaji na serikali,kujenga viwanda vya nyama na maziwa pamoja na kutatua migogoro ya ardhi iliyodumu kwa muda mrefu kati ya wananchi wanaopakana na Ranchi za Taifa.

Alisema Pamoja na Serikali kuweka mikakati mizuri inayoendelea kuwekwa bado kuna changamoto mbalimbali ikiwemo wawekezaji kutolipa kodi kwa wakati ambapo wawekezaji wa Kagera wanadaiwa kiasi cha sh. Bilion 1.1, vikao vya ujirani mwema kutofikia hitimisho na baadhi ya wafugaji kutoka nchi jirani kuvamia maeneo.

Mbunge wa Jimbo la Nkenge, Balozi Diodorus Kamalaambaye ni mjumbe wa kamati ya bajeti alitoa shukrani kwa Serikali kutatua mgogoro uliodumu kwa miaka 12,ambapo wananchi wa Kata Kakunyu walio karibu na Ranchi ya Missenyi walikosa maeneo ya kuishi na kuvunjiwa maeneo yao na sasa wamepata maeneo mengine yaliyotengwa na serikali.

Wawekezaji hao waliohudhuria kikao cha kamati ya Bunge pamoja na kutoa Shukurani kwa Serikali kwa kuwajali na kuwapa maeneo ya kuweka wamelalamikia utitiri wa kodi . Waliiomba Serikali kuwapatia taarifa kuhusu upatikanaji wa masoko ya kuuza nyama nje ya nchi.

MAJIRA UK 7.

Scanned by CamScanner

# Wavuvi Kagera washauri sheria ibadilishwe

**Na Ashura Jumapili, Bukoba**

WAVUVI na wafanyabiashara wa mazao ya samaki mkoani Kagera wameiom ıa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo,Mifugo na Maji kuishauri Serikali kubadilisha sheria namba 22 ya uvuvi ya mwaka 2003 kwa madai kuwa sheria hiyo ni kandamizi imewafanya baadhi ya wafanyabiashara kuhamia nchini Uganda.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye kikao cha kamati hiyo na kilichofanyika katika ukumbi wa mkuu wa mkoa wa Kagera wavuvi hao walisema umefika wakati wa kubadilisha sheria ya uvuvi na kutunga sheria mpya yenye maslahi mapana kwa wavuvi na wafanyabiashara.

Medard Kaijage ni mvuvi alisema Nyavu za (single )zinazotakiwa kutumika kwa mujibu wa sheria za uvuvi hapa nchini watu wanapoenda kuvua hawapati samaki na badala yake watu wanatumia makokoro na nyavu ndogo.

Kaijage,alisema hata wakikamatwa na vikosi vya doria bado wanaendelea kutumia makokoro kwa sababu bei yake ni ndogo yanauzwa kati ya sh. 200,000 hadi 500,000 na kudai kuwa wanafadhiliwa fedha na wafanyabiashara wakubwa.

Alisema kokoro ni hatari kutumika katika uvuvi kwa sababu kwanza yanaharibu na mazalia ya samaki yakipelekwa Ziwani mara moja yanakuja na samaki wadogo ambao havijakomaa kama gunia tano na wakati mwingine wanashindikana kuuzika wanalazimika kufukia chini ya mchanga.

Alisema nyavu ya dabo inayokataliwa inavua samaki wanaokubalika na ndio maana Uganda wao wanajali saizi ya jicho na ukikutwa unatumika kokoro unapigwa risasi.

"Mtuhurumie kwenye uvuvi tuweze kufanya biashara na tulipe kodi sheria kandamizi zinatutia umasikini," alisema Kaijage.

Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah,alisema tatizo kubwa la wavuvi wa Tanzania ni kutokuwa na mitaji, hivyo Waganda wanatumia mwanya huo kuwapa mitaji na samaki wanapelekwa kwao.

Tamatamah,alisema wavuvi wa Tanzania wana soko Uganda kwa sababu wanasifiwa kuwa ni wazuri.

Alisema viwanda vya Uganda ni vidogo sio vikubwa kama Tanzania ndio maana gharama za uendeshaji huko ziko chini. Alisema wao hawakati minofu wanasafirisha samaki jinsi alivyo akiwa freshi na kudai kuwa Tanzania wanazuia kutumia nyavu za dabo lakini Uganda wanazitumia.

"Tozo ni kubwa mfano kilo moja ya mabondo wilaya ya Muleba inatozwa sh. 4,000 wakati mwingine mfanyabaishara analazimika kulipa ili mzigo wake usiharibike,"alisema Dkt. Tamatamah.

Alisema viwanda vya samaki vinasaidia sana katika soko la ajira kwa wa Watanzania. Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo,mifugo na maji Pascal Haonga,alisema sheria za uvuvi zinatungwa na nchi kwa kushirikiana na nchi jirani.

# Kamati ya na Wakala

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Mazingira, imeipongeza Wakala wa Vipimo WMA kwa kufanya kazi kisasa zaidi hasa kwenye kituo hicho cha Misugusugu. Pongezi hizo zilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Suleiman Sadiq Murad, wakati Kamati hiyo ilipotembelea kituo cha ukagauzi wa mita za maji na matenki ya mafuta kilichoko Misugusugu Mkoa wa Pwani.

Alisema WMA imefanikiwa kuzifanyia kazi changamoto ambazo wabunge walizitoa wakati Kamati hiyo ilipokutana na maofisa wa wakala mwaka



# Serikali kuv

**Na Ashura Jumapili, Missenyi**

SERIKALI kupitia Wizar
Mifugo na Uvuvi ipo tayari kuwa
wawekezaji wazawa waliowe
katika Ranchi za Taifa (NAR
kupata mikopo katika taasis
fedha kwa kutumia mifugo y
waweze kufanya uwekezaji w
tija na kuinua sekta hiyo. Kauli
ilitolewa na Naibu Waziri wa K
na Mifugo, Abdallah Ulenga n
ya Kamati ya Kudumu ya B
ya Kilimo,Mifugo na Maji
tembelea MARCO wilayani M
na kuzungumza na wawekeza
wazawa waliowekeza eneo
Ulenga alisema miaka
wafugaji wanashindwa kukop
sababu mifugo haipokelewi

Scanned by CamScanner